

Jumamosi terehe 21 mwezi wa 5, 2022

Natuma salaam kwa jamii yote ya wasome wa mashule ya serikali mjini Buffalo (BPS)

Juma iliyopita, kulikuwa tokeo lililotuletea huzuni na usumbufu kubwa sana sisi wote katika mashule ya serikali mjini Buffalo. Tokeo hili lilituletea kiwewe na tukawa kwa msiba usiwoweza kufasiriwa, watu wema kumi walipouwawa kiholela.

Chuki ya aina yoyote ni kama sumu, na hatuwezi kuyivumulia kamwe, katika vituo vya mashule yetu. Nawaomba watumishi wote wa BPS, wanafunzi, familia na jamii ya wasome kwa jumla, kutowa repoti, baada ya kupata lisala yoyote ya chuki. Ni muhimu sana kuelewa kwamba kunyamaza iko kama kuwa mushiriki wa kitendo cha ufidadi. Maombi yangu ni haya: “ukiona, au ukisikia mpango wa kitendo cha ufidadi...toa taarifa...mbio!” Usisimame hapo na kufikiri kwamba mtu mungine ndiye atatoa taarifa. **TUNAAMRISHWA KUWA WASHIRIKI WA MAPINDUZI; TUNATAKA WOTE KUONA!** Tunalazimishwa kufanya hivi, kwa kuzingatia miaka ijayo ya watoto wetu!

Wiki iliyopita, tuliona pia uungwana mkubwa, na jamii kujiunga pamoja katika mjyi wetu wa “ujirani mwema”, kama sijaona mimi hapo mbele! Tabia hii ilituletea tumaini kubwa kwa maisha ya hapo baadaye, hata katika wakati huu tulipozama ndani ya kihoro.

Nataka niwajulishe kwamba nilisikia fahari sana kwa kuona jinsi watumishi wa BPS waliposimana imara. Kila mmojal Wiki iliyopita, muliungana kwa kutoa huduma, kwa kutoa elimu, na kwa kuwaunga mkono wanafunzi wetu mukiendelea kusikitishwa ndani kwa sababu ya huzuni ya msiba huu. Uweledi wenu pamoja na masikitiko moyoni niyojionea mwenyewe vinawafanya kuwa watumishi wa daraja la juu! Nawashukuru sana!!

Kwa wanafunzi wetu na familia za BPS: nawaomba muendeleo kuonesha uvumilivu, imani na ushupavu. Najua kuwa wiki hii ilikua mbaya; ilikua na tishio na iliwaachia hisia za wasiwasi... na haingekua namna tofauti! Lakini, pamoja na hayo, muliweza kuonesha nchi yetu nzima kwamba ELIMU NU MUHIMU, na kuwa hatutaruhusu vitendo vya kinyama na chuki kuvuruga lengo letu katika BPS. Nilipendezwa sana na mwenendo wenu. Tunajua kuwa muna tumaini na ndoto za maisha mema na faida kubwa hapo baadaye; na sisi kama walezi, tunazingatia mamlaka yetu kwa dhati, ya kusaidia kila mwanafunzi kufika kwa shabaha yake.

Kwa kumaliza, kwa mashule yetu, na kwa washiriki wetu wote katika jamii: mulisimama bega kwa bega pamoja na si, mukaonesha mfano wa ushirikiano wa kweli! Asante kwa kuitika muto wa wajibu na kwa kuleta msada uliwohitajiwa kwa roho nzuri, ili kuunga mkono wanafunzi, watumishi wa mashalwe yetu... NA TUNAEENDELEA KUPANDA JUU!

Wenu awapendaye,

Dr. Tonja M. Williams, Kiongozi mkuu wa muda wa mashule

Nakala halisi kwa: Washiriki wa halmashauri kuu ya elimu